TANGAZO LA SERIKALI NA. 275 tarehe 7/4/2023

SHERIA YA OFISI YA TAIFA YA MASHTAKA,

(SURA YA 430)

# NOTISI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 22)*

NOTISI YA UTEUZI WA WAENDESHA MASHTAKA YA MWAKA 2023

Jina

1. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Uteuzi wa Mwendesha Mashtaka ya Mwaka 2023.

Uteuzi wa mwendesha mashtaka

2. Mtu ambaye jina lakelimetajwa katika Jedwali ameteuliwa kuwa mwendesha mashtaka kwa madhumuni ya kuendesha mashauri ya jinai kwa niaba ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

Uhalali wa uteuzi

3.-(1) Uteuzi wa mwendesha mashtaka chini ya aya ya 2 utakuwa halali kwa kipindi cha miaka mitano kutoka tarehe ya kuanza kutumika kwa Notisi hii.

(2) Bila kujali masharti ya aya ndogo ya (1), mtu aliyeteuliwa chini ya Notisi hii anaweza kutumikia nafasi hiyo kwa kipindi kinachopungua miaka mitano endapo ajira ya mtu huyo kwenye Utumishi wa umma itakoma au uteuzi wa mtu huyo utaamuliwa vinginevyo na Mkurugenzi wa Mashtaka.

/

*Tangazo la Serikali Na. 275 (linaendelea)*

**JEDWALI**

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

| NA. | JINA |
|---|---|
| 1. | Reteti Repilal Molloimet |

Dodoma,
16 Machi, 2023

SYLVESTER ANTHONY MWAKITALU
*Mkurugenzi wa Mashtaka*